

'Pedi' zinazotumika miaka mitatu zavumbuliwa

MWANDISHI WETU

MWANAFUNZI Zyaan Virji (16), amevumbua taulo za kike (pedi) zenye uwezo wa kutumika kwa miaka mitatu hadi mitano.

Pedi hizo zinatengenezwa kwa ajili ya kuwarahisisha wasichana wasiokuwa na uwezo wa kununua zinazouzwa bei kubwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa pedi hizo uliofanyika jana jijini Dar es Salaam, Virji alisema zitauzwa kati ya shilingi 12,000 hadi 15,000.

Alisema mfuko mmoja utakuwa na pesi nane, taulo na sabuni hivyo mtumiaji kuzisafisha na kurudia kuzitumia kwa kipindi cha kati ya miaka mitatu hadi mitano.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Waziri wa zamani wa viwanda, Shamim Khan ambaye alimpongeza

Virji kwa kubuni pedi hizo na kuwataka vijana wengine kuiga mfano huo.

Virji ambaye ni kijana wa kiume na mwanafunzi wa Shule ya Agha Khan, alisema sababu zilizomsukuma kubuni pedi za aina hiyo ni gharama kubwa ya zilizopo sasa sokoni ambazo kwa Mtanzania mwenye kipato cha chini ni vigumu kuzinunua. Alisema alianza kwa kufanya utafiti na kubaini idadi kubwa ya wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini wanapata shida wakati wa hedhi, hususan baadhi ya wanafunzi wasiokuwa na uwezo.

Alisema wanafunzi wasiokuwa na uwezo wa kununua pedi zinazouzwa gharama kubwa wamekuwa wakishindwa kuhudhuria masomo kwa muda wanaokuwa kwenye hedhi.

Alipoulizwa sababu iliyomsukuma yeye kijana wa kiume kubuni pedi hizo Virji alijibu; "siku moja katika pitapita

zangu madukani nikaona moja kati ya bidhaa za hedhi ikiuzwa kwa bei ghali, nikajikuta niingiwa na maswali mengi, ni nini ambacho kinafanya taulo hizi kuuzwa ghali hivi?

"Hivi wasichana na wanawake wenye hali ngumu wataweza kumudu kama tu baadhi yao wanashindwa kujikimu kwa mlo wa kila siku watawezaje kutoa fedha kwa ajili ya kujinunulia pedi?," alihoji

Alisema maswali hayo ndiyo yalimfanya apate wazo la kuzindua taulo ambazo zitakuwa na bei ya chini na zenye uwezo wa kudumu kwa kipindi kirefu. Kabla ya kutengeneza pedi hizo ambazo bado hazijapewa jina, Virji alifanya tafti katika shule mbalimbali na kubaini kuwa asilimia mbili ya wanafunzi ndiyo wenye uwezo wa kumudu kununua pedi zilizoko sokoni kwa sasa.